Maisha yangu

Kazi yangu

Kazi yangu salama

Kudhibiti Hatari katika Mazingira ya Kazi

Siku ya Usalama na Afya Kazini Duniani

maisha

kazi

kazi salama

www.ilo.org/safework/safeday

28 Aprili, 2008

[ISSA logo]

Siku ya ILO ya Usalama na Afya Kazini Duniani kwa kuungwa mkono na ISSA

Siku ya ILO ya Usalama na Afya Kazini Duniani

Hakimiliki © International Labour Organization 2008

Chapa ya kwanza 2008

Machapisho ya Shirika la Kazi Duniani yanalindwa na hatimiliki chini ya kanuni ya 2 ya Mkataba wa Hakimiliki wa Kimataifa. Hata hivyo, nukuu fupi zinaweza kutumiwa bila kuomba kibali ilimradi chanzo cha nukuu hizo kionyeshwe wazi wazi. Lakini mtu anayetaka kurudufisha au kutafsiri Machapisho ya ILO sharti aombe kibali kutoka kwa Taasisi ya Uchapishaji (Haki na Vibali), Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani, CH-1211 Geneva 22, Switzerland, au kwa barua-pepe: pubdroit@ilo.org. Shirika la Kazi Duniani linakaribisha maombi kama hayo.

Maktaba, taasisi na watumiaji wengine waliosajiliwa na mashirika yanayotoa haki ya kurudufu wanaweza kutoa nakala kulingana na leseni walizopewa kwa madhumuni hayo. Tazama www.ifrro.org ili kupata shirika linalotoa haki za kurudufu katika nchi yako.

ISBN [...] (print)
ISBN [...] (web pdf)
Pia kinapatikana kwa lugha ya Kifaransa: Ma vie, mon travail, mon travail en sécurité - Gestion du risqué en milieu de travail (ISBN …), Geneva, 2008, in Spanish : Mi vida, mi trabajo, mi trabajo en seguridad - Gestión del riesgo en el medio laboral (ISBN ...), Geneva, 2008.

Katalogi za ILO katika Orodha ya Machapisho

Maelezo yaliyotumika katika machapisho ya ILO, ambayo yanazingatia taratibu za Umoja wa Mataifa pamoja na mfumo wa mpangilio uliotumika ndani ya machapisho hayo havitoi msimamo

wowote wa Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani kuhusiana na hadhi ya kisheria ya nchi yoyote, eneo au kanda yoyote au viongozi wake, au kuhusiana na mipaka ya maeneo hayo.

Majukumu kuhusiana na mawazo yaliyotolewa katika makala zilizosainiwa, tafiti au michango mingine ya maandishi yanabebwa na waandishi wenyewe na wala Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani haichukui jukumu lolote kuhusiana na mawazo yaliyotolewa ndani yake kutokana na kuwa mchapishaji wa maandishi hayo.

Marejeo ya majina ya makampuni na bidhaa za kibiashara pamoja na michakato mbali mbali haina maana kwamba Ofisi ya Shirika la Kazi Duniani inakubaliana nayo wala kukosa kutaja kampuni mahususi, bidhaa ya kibiashara au mchakato fulani hakumaanishi kwamba ILO haitambui viro hivyo.

Machapisho ya ILO yanaweza kupatikana kupitia maduka makubwa ya kuuza vitabu au kutoka ofisi za ILO katika nchi yoyote ile, au moja kwa moja kutoka “ILO Publications, Intemational Labour Office, CH-1211 Geneva 22, Switzerland”. Aidha katalogi au orodha za machapisho mapya zinapatikana na kutolewa bure kupitia anwani hiyo iliyotolewa, au kwa barua pepe: pubvente@ilo.org.

Angalia mtandao wetu: www.ilo.org/publns
Kimechapishwa [nchi]

Siku ya Usalama na Afya Kazini Duniani Tarehe 28 Aprili 2008

The Daily W

Thursday, 24 April 2008

My life, My Work, My Safe

Managing Risk in the Work Environment

"Last week's tragedy in which our town lost four brave coal miners showed us all how important the problem of risks at work can be. Events such as these force us to examine the risks related to our own jobs. For this article, I intended to profile some of the risks facing local workers, but I need look no further than my own work to find many opportunities to reduce risk..."

SHIRIKA LA KAZI DUNIANI, GENEVA
Siku ya Usalama na Afya Kazini Duniani Tarehe 28 Aprili 2008

Maisha Yangu, Kazi Yangu, Kazi Yangu Salama
Kudhibiti Hatari katika Mazingira ya Kazi

Wachimba Migodi Wafa Kutokana na Mlipuko

Hatari hizi zilikuwa zinawezekana kuepukwa?

Kulikuwa na njia nyingine ya kufanya kazi ambayo ingepunguza, kama si kuondoa, matatizo yaliyosababisha janga hili?

Nini kifanyike ili kuhakikisha kuwa janga kama hili halitokei tena?

Mbali na juhudi kubwa za kupunguza ajali na magonjwa katika migodi kama ilivyo kwenye sekta nyingine, kuumia na magonjwa bado ni matukio ya kawaida katika ulimwengu wa kazi hadi leo.

Waraka huu unaeleza baadhi ya hatua za msingi za kudhibiti hatari kazini.

Hatari Kazini

NANI?

Watu kila mahali wanakuwa kwenye mazingira hatari kwa usalama na afya kutokana na kazi zao.

Mnamo mwaka 2005, Shirika la Kazi Duniani (ILO) lilikadiria kuwa duniani kote watu milioni 2.2 hufa kila mwaka kutokana na ajali na magonjwa yanayohusiana na kazi. Na vifo vinavyohusiana na kazi vinaonekana kuongezeka. Zaidi ya hayo, kila mwaka inakadiriwa kuwa hutokea ajali milioni 270 zizizosababisha maafa zinazohusiana na kazi (kila moja ikiwa imesababisha kushindwa kufika kazini kwa angalau siku tatu) na vilevile matukio milioni 160 ya magonjwa yanayohusiana na kazi. Usalama na afya kazini

ni tatizo la serikali, waajiri, wafanyakazi na familia duniani kote. Ingawa baadhi ya tasnia zina madhara kuliko nyingine, makundi kama vile wakimbizi au wafanyakazi wengine wanaoishi katika mazingira magumu mara nyingi huwa katika hatari ya kupata ajali na magonjwa yanayohusiana na kazi, kwa kuwa umaskini mara kwa mara huwalazimisha kujiingiza kwenye kazi zisizokuwa salama.

Miriam ni mwandishi wa habari mwenye uzoefu anayefanya kazi katika gazeti la kila siku mjini. Siku moja, Mhariri Mkuu alimteua kuchukua hotuba ya Waziri wa Kazi iliyopangwa kutolewa kwa ajili ya Siku ya Usalama na Afya Kazini Duniani tarehe 29 Aprili. Mhariri alimtaka Miriam kufuatilia makala ya siku iliyopita kuhusu kifo cha wachimbaji wanne wa makaa ya mawe. Miriam alimuuliza Waziri wa Kazi baadhi ya maswali kuhusu nafasi ya serikali katika ukaguzi na uendelezaji wa mifumo ya ndani ya usimamizi ambayo hubainisha, kuzuia na kupunguza hatari katika migodi ya ndani ya nchi, ili majanga haya yasiwe chanzo cha maafa mengine. Miriam alimwita mkaguzi wa migodi na kumuuliza maswali yanayohusu nafasi ya serikali katika uzuiaji wa ajali. Mkaguzi alimweleza kuwa ingawa maisha yamejaa hatari nyingi, mambo mengi yangeweza kufanyika kuondoa au kupunguza uwezekano wa kutokea madhara.

Wakati wa mahojiano na mkaguzi, Miriam alijifunza kuhusu “mpangilio wa vidhibiti” kwa ajili ya kumudu hatari kazini kwa kufuata utaratibu wa hatua nne:

1. Kuondoa au kupunguza hatari kwenye chanzo;
2. Kupunguza hatari kwa kutumia udhibiti wa kihandisi au kinga nyingine;
3. Kuweka taratibu salama za kufanya kazi ili kupunguza hatari zaidi, na
4. Kugawa, kuvaa na kutunza vifaa vya kujikinga.

Aligundua kuwa kanuni hizi zilizoandaliwa vizuri tayari zimeshaingizwa kwenye sheria nyingi za nchi na viwango vya kimataifa, ili kuonyesha msimamo wa nchi nyingi wa kuboresha usalama na afya kwa wafanyakazi wote.

Miriam alijifunza kuwa Waziri wa Kazi alionyesha msimamo kwa kuchukua hatua za kuridhia Mfumo wa Kuendeleza Mkataba wa Usalama na Afya Kazini wa Shirika la Kazi Duniani, 2006. Mkataba huu umeweka mkakati mmoja wa kuandaa mfumo wa kitaifa wa kuongeza ufanisi wa mfumo wa taifa wa usalama na afya. Ikiwa kama hatua ya kwanza, Waziri aliagiza Idara ya Usalama na Afya Kazini kufanya kazi ya maandalizi ya mpango wa usalama na afya kazini kitaifa kwa kushirikiana na idara nyingine za serikali na washirika wa kijamii.

Waziri pia alikuwa ashiriki kwenye Kilele cha Masuala ya Usalama na Afya katika Mkutano Maalum wa Usalama na Afya Kazini hapo Juni 2008 (tazama hapo chini). Huu ulitakiwa kuwa mkutano wa kwanza wa viongozi wa ngazi za juu na Mawaziri, Maafisa Waandamizi na vyama vya wafanyakazi duniani juu ya usalama na afya kazini.

Kuchunguza taarifa kuhusu kuzuia hatari katika migodi kulibadili mtazamo wa Miriam juu ya usalama na afya mahali pa kazi. Alianza kuangalia hali yake na kuanza kuchunguza njia za kupunguza hatari zake mwenyewe. Aliangalia kurasa za Tovuti za mashirika ya waajiri kama vile Chama cha Wamilki wa Magazeti Duniani, vyama vya mashirika ya utangazaji, vyama vya wafanyakazi na serikali katika kujaribu kupata kinga ya afya kazini kama mwandishi wa habari.

Miriam aligundua kuwa waandishi wa habari wanaweza kuuweka usalama wao hatarini ili kutuletea habari kutoka katika nyanja za majanga ya kiekolojia au ajali za viwandani, kama vile umwagikaji wa kemikali au milipuko ya migodi au maeneo ya vita. Vurugu kazini ni hatari nyingine inayowakabili.

Kamati ya Kuwalinda Waandishi wa Habari imeripoti kuwa zaidi ya waandishi wa habari 660 waliuawa katika kipindi cha miaka 15 iliyopita, na Taasisi ya Kimataifa ya Usalama wa Wanahabari na Chama cha Wamiliki wa Magazeti Duniani vimeweka msimamo wa kuendeleza usalama wa waandishi wa habari. Azimio la 1736 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (2006), limethibitisha: “Linasikitishwa sana na matukio mengi ya vurugu katika maeneo mengi duniani dhidi ya waandishi wa habari, wataalamu wa vyombo vya habari na wafanyakazi wa vyama ….. waheshimiwe na kulindwa ipasavyo …..”. Alishangaa kuona kuwa siku nyingi tangu mwaka 2000, Shirika la Kazi Duniani lilishafanya mikutano kujadili athari za teknolojia ya habari kwa uandishi wa habari na mnamo 2006, Azimio la 1736 la Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa lililaani vikali mauaji ya waandishi wa habari.

Kwa kuangalia kwa mtazamo wa kuzuia na kupunguza hatari yake kazini, na kuwezeshwa na serikali pamoja na jamii ya kimataifa kwa kupatiwa maarifa ya mifumo ya taaluma yake, mwandishi ametambua mapema kuwa mifumo ipo kumsaidia kudhibiti hatari kazini. “Nilijua kulikuwa na matatizo ambayo yangeweza kuathiri afya yangu kazini, lakini sikuwahi kufikiri kuwa mtu mwingine yeyote ameyafanyia uchunguzi,” alifikiri.

Na hivyo aliandika:
“Janga la wiki iliyopita ambapo mji wetu ulipoteza wachimbaji wanne shupavu wa makaa limetuonyesha sote kuwa tatizo la hatari kazini lina umuhimu kiasi gani. Matukio kama haya hutulazimu kuchunguza hatari zinazohusiana na kazi zetu. Kwa makala haya, nilikusudia kutoa maelezo mafupi ya baadhi ya hatari zinazowakabili wafanyakazi wa kawaida, lakini nimegundua kuwa sihitaji kuangalia mbali zaidi ya kazi yangu mwenyewe kuona fursa nyingi za kupunguza hatari …..”

NINI?

Mameneja na wafanyakazi wote wanahitaji kujua kuhusu jinsi ya kudhibiti na kupunguza hatari katika sehemu zao za kazi, kuzuia kuumia na kulinda usalama na afya zao.

Ajali na magonjwa kazini mara nyingi huchangiwa na sababu mbalimbali; zikiwemo sababu za kiasasi, kimaumbile na kibinadamu. Hatari zinaweza kuainishwa kwa njia mbalimbali, kama vile:

- kulingana na aina, kwa mfano:
  - mitambo
  - kemikali
  - mazingira na
  - hatari za kisaikolojia na kijamii,
- au kulingana na madhara yaliyotokea, kwa mfano:
  - kuharibikiwa uwezo wa kusikia kutokana na kelele kubwa
  - vidonda kutokana na ajali za mashine na
  - matatizo ya viungo kutokana na kuumia

baadhi ya viwanda husababisha hatari mbalimbali. Kwa mfano, katika migodi, wafanyakazi kuendesha kifaa kinachokwenda kasi katika mazingira yenye mwanga hafifu, mara kwa mara kuwa katika mazingira hatari ya vumbi jingi na harufu mbaya na kukumbana na hatari ya milipuko au mwako utokanao na kemikali.

KWA NINI?

Kudhibiti hatari katika mazingira ya kazi hupunguza athari za kibinadamu na kiuchumi za ajali na magonjwa yanayohusiana na kazi.

[Ingiza picha ya mchomeaji (e3944)]

Ajali na magonjwa yanayohusiana na kazi huweka mzigo kupita kiasi wa kibinadamu na kiuchumi kwa wafanyakazi na familia zao na vilevile kwa biashara na jamii kwa ujumla. Shirika la Kazi Duniani hivi karibuni limekadiria kuwa gharama za kiuchumi kutokana na ajali na magonjwa yanayohusiana na kazi duniani zimefikia sawa na 4% ya zao la ndani duniani – zaidi ya mara 20 ya msaada wa maendeleo. Kinyume chake, kuna ushahidi ulio wazi kuwa nguvukazi yenye afya huongeza uzalishaji katika biashara na kuzipatia biashara faida na uchumi wa kitaifa kwa kupunguza idadi ya ajali na magonjwa na kupunguza idadi ya madai ya bima na fidia.

VIPI?

Mbinu za kudhibiti hatari zinabainisha, zinatoa matarajio na kutathmini madhara na hatari na kuchukua hatua madhubuti kudhibiti na kupunguza hatari.

Hatua ya kwanza kwenye mchakato ni kubainisha madhara katika mazingira ya kazi na kutathmini hatari za kuumia zinazohusiana nazo, ama za ajali au ugonjwa. Ili kuekeleza hili, mara nyingi ni muhimu kuangalia vyanzo vinavyoaminika vya habari, kama vile maelekezo ya wazalishaji na vyanzo vingine vya ushauri bora. Ni muhimu kuchunguza kama mipango na tahadhari zilizopo zinatosha au hazitoshi kudhibiti au kupunguza hatari. Kama hazitoshi hatua zaidi zichukuliwe kufanya hivyo, kwa kufuata mpangilio wa vipaumbele kama ifuatavyo.

Hatua nne za muhimu kupunguza hatari

1. Kuondoa au kupunguza hatari kwenye chanzo

Hii ni hatua ya kwanza muhimu inayokusudia kuondoa au kupunguza hatari kabla hazijaingia mahali pa kazi. Wazalishaji na wasambazaji wa vifaa vya kazi na kemikali waeleze mikabala ya kiubunifu kutatua matatizo haya. Kwa mfano, inawezekana kubadili kemikali yenye madhara makubwa zaidi na kemikali yenye madhara kidogo zaidi ambayo itatimiza malengo yanayofanana. Asbesto ni dutu hatari sana, ambayo imepigwa marufuku kutumika katika nchi nyingi, lakini inaweza kubadilishwa na vifaa vingine mbadala vilivyo salama zaidi. Mfano mwingine, ni utoaji wa kelele na mitetemo unaofanywa na vifaa vya kazi unaweza kupunguzwa zaidi kwa kuwa miundo bora katika hatua za uzalishaji.

2. Kupunguza hatari kwa kutumia udhibiti wa kihandisi au vizuizi vingine

[ingiza picha ya maabara ya tiba (c0330)]

Iwapo hatari zinaweza au haziwezi kuondolewa au kupunguzwa katika chanzo, mara nyingi zinaweza kuendelea kupunguzwa kwa kutumia vifaa maalum. Hii inaweza kufanywa kwa urahisi zaidi – kuweka reli za kuzuia kuanguka katika ngazi za kwenye jukwaa au vifaa vya kufunika kuzuia vifaa vya umeme. Mzunguko mzuri wa hewa pia hutoa kinga dhidi ya hatari ya dutu zenye madhara, kwa mfano, kama ilivyo kwenye chumba cha upasuaji hospitalini, ambapo wauguzi na madaktari wanatakiwa kupatiwa kinga dhiri ya hewa za dawa za kulevya. Udhibiti wa kihandisi kama huo unatakiwa kuwekwa ipasavyo ili uendelee kufanya kazi, na ni muhimu taratibu za kufanya matengenezo zifanywe kuwa sehemu ya mfumo mzima wa usimamizi wa usalama na afya kazini.

3. Kuweka taratibu salama za kufanya kazi ili kuzidi kupunguza hatari

Upangaji mzuri wa mipango na taratibu wakati wote ni muhimu hasa kwa baadhi ya shughuli. Kwa mfano, kazi ya matengenezo au uzibuaji katika mashine iliyoziba inahitaji kufuata utaratibu salama wa kufanya kazi mahali bila kuwepo mtu mwingine ili kuzuia mashine isiweze kuwashwa kwa bahati mbaya; wafanyakazi wengi wamekuwa wakiumia wakati wa shughuli kama hizo. Kufanya kazi katika mnururisho wa ioni pia unahitaji mipango na taratibu makini, kama vile beji au vyombo vya kuzuia mnururisho kuvaliwa na wale wanaofanya kazi hizo na kutumia vizuizi sahihi. Alama na ishara za kuonya pia ni hatua za kuzuia zinazofaa, lakini zinahitaji kutumiwa pamoja na tahadhari nyingine na zinafaa tu kama zitakuwa zinaonekana au kusikika na katika lugha inayoeleweka kwa kila mmoja.

4. Kugawa, kuvaa na kutunza vifaa binafsi vya kujikinga

[ingiza picha ya wazimamoto (e0088)]

Kugawa vifaa vya kujikinga, kama vile barakoa ya kuzuia vumbi na vifaa vya kupunguza ukali wa sauti masikioni, ni kinga inayoaminika kidogo zaidi kwa kuwa ufanisi wake unategemea uchaguzi sahihi, mafunzo, matumizi na utunzaji. Hivyo, **vifaa vya kujikinga vitumike kama njia ya mwisho.** Hata hivyo, vifaa hivi vinahitajika kwa baadhi ya shughuli. Kwa mfano, mzunguko mzuri wa hewa hauwezi kuwakinga wazimamoto katika dharura. Vilevile, vifaa vya kuzuia makelele vinaweza kuvaliwa na wale wanaofanya kazi katika mazingira yenye makelele, hata kama njia nyingine zimetumika kwa mafanikio kupunguza sauti iwezekanavyo. Vifaa vya kujikinga vinahitaji kuwa vya kuwafaa wafanyakazi husika na kutunzwa ipasavyo ili viendelee kufaa.

Kudhibiti hatari kazini

Udhibiti wa usalama na afya kwa ufanisi unahitaji kuwepo utaratibu unaoungwa mkono vya kutosha pamoja na majukumu

yaliyo wazi ya usalama na afya na taratibu za kushughulikia hatari. Hii inajumuisha kutoa mafunzo na taarifa muhimu na kusimamia wafanyakazi wapya au vijana. Kwa kuwa mazingira ya kazi yanaweza kubadilika kila siku, usalama na afya unahitaji uangalifu wa mara kwa mara. Viashiria kama vile viwango vya kuumia, ugonjwa na kukosa kufika kazini vinaonyesha kama usalama na afya unadhibitiwa vizuri kwa vitendo au hapana. Maelezo zaidi kuhusu jinsi ya kudhibiti usalama na afya kazini yametolewa katika *Mwongozo wa mifumo ya usimamizi wa usalama na afya kazini*, ILO, 2001.

Majukumu ya Pamoja …. Mfanyakazi, mwajiri, serikali na jamii

Kila mmoja ana jukumu la kutekeleza ili kufanya mahali pa kazi kuwa penye usalama na afya iwezekanavyo.

Waajiri na wafanyakazi

Mkataba wa Shirika la Kazi Duniani wa Usalama na Afya Kazini, 1981 (Na. 155) unaeleza kuwa waajiri wanatakiwa kuhakikisha kuwa, kwa kadiri inavyowezekana, mahali pa kazi, vifaa na dutu ni salama na bila kuwepo hatari kwa afya. Hivyo, hatari zote za mahali pa kazi, iwe za vifaa, kemikali au kimaumbile, zinatakiwa kudhibitiwa ipasavyo. Wafanyakazi wote wapatiwe maelezo na mafunzo wanayohitaji. Nguo na vifaa vya kujikinga vinapohitajika, pia vitolewe bure.

Wafanyakazi wapatiwe wakati wote:

- ✓ Mafunzo kuhusu hatua za kuzuia
- ✓ Maelezo mara kwa mara, kuhusu hatari fulani katika kazi zao
- ✓ Wapatiwe maelezo kuhusu madhara ya jumla mahali pao pa kazi

kuhusu:

- ➢ Madhara kwa mwili kama vile makelele, joto lisilokuwa sahihi au mwanga duni

- Dutu hatari za kemikali na kibiolojia na athari zake mbaya
- Sababu za kisaikolojia na kijamii

Chini ya viwango hivyo vya kimataifa, wafanyakazi washirikiane na waajiri katika kutimiza wajibu waliopewa na kuripoti hali ambazo zinaleta hatari karibu. Wafuate maelekezo yaliyotolewa kwa ajili ya usalama na afya yao na wengine.

Serikali

Serikali zinawajibika kutunga sera za kitaifa kwa ajili ya usalama na afya kazini na kuweka mfumo wa ukaguzi wenye ufanisi na utekelezaji wa sheria husika. Viwango vya kazi vya kimataifa viridhiwe na kutekelezwa kwa kiwango kinachowezekana. Serikali pia zikusanye taarifa husika za takwimu kuhusiana na ajali na magonjwa kazini, kupima maendeleo katika kuelekea kwenye malengo ya kitaifa na kutoa taarifa kwa watunga sera wa siku za baadaye.

Elimu, mafunzo na utafiti

Taasisi za elimu na mafunzo zina nafasi muhimu katika kuamsha ufahamu wa hatari zinazohusiana na kazi na jinsi zinavyoweza kudhibitiwa ipasavyo. Katika baadhi ya nchi, elimu juu ya hatari kwa sasa ni sehemu ya mtaala wa shule kitaifa, kuwawezesha watoto kujifunza kuhusu hatari zinazohusiana na kazi kabla hawajamaliza shule. Vyuo vikuu na taasisi za utafiti zinachukua nafasi muhimu, kwa kuwa zinafanya uchunguzi wa hatari, vinaweka msingi unaofaa wa kiufundi na kisayansi kwa ajili ya kufanya tathmini na usimamizi wa hatari na kuandaa njia za kibunifu za kupunguza hatari (kama zile zinazotokana na kuanzishwa kwa teknolojia mpya).

Jamii ya kimataifa

Mashirika mengi ya kimataifa yanashiriki kikamilifu katika kuhamasisha usalama na afya kazini.

Ajenda ya Shirika la Kazi Duniani ya Kazi Zenye Staha imezingatia uelewa kwamba kazi ni chanzo cha kuheshimiwa, mshikamano wa familia, amani katika jamii, demokrasia ambayo inajali watu na ukuaji wa uchumi ambao huongeza fursa ya kazi zenye kuleta kipato na maendeleo ya biashara. Uhamasishaji wa usalama na afya kazini ni moja ya njia za kufanya Kazi Zenye Staha ziwezekane duniani.

Shirika la Kazi Duniani limepitisha viwango vingi vya kimataifa kuhusu suala hili, ambavyo vinaingiza sekta mbalimbali na madhara halisi. Uzuiaji wa hatari ni kiini cha viwango hivi na umeingizwa ndani ya Mkataba wa Kukuza Mfumo wa Usalama na Afya Kazini, 2006 (Na. 187) na Mapendekezo yake (Na. 197), ambayo yanajaribu kukuza utamaduni wa kinga ya usalama na afya na mifumo ya usimamizi wa afya na usalama kupitia sera, mifumo na programu za kitaifa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

International Programme on Safety and Health at Work and Environment (Safework)

Simu: +41.22.779.6715

Faksi: +41.22.799.6878

Barua-Pepe: safework@ilo.org

www.ilo.org/safework/safety

Mkutano wa XVIII Duniani juu ya Usalama na Afya Kazini
Mkutano wa Dunia kwa ajili ya Kinga

Usalama na Afya Kazini: Wajibu wa Kijamii
Juni 29 – Julai 2, 2008
COEX Convention Center, Seoul, Korea

Mkutano wa XVIII Duniani juu ya Usalama na Afya Kazini unatoa fursa ya kipekee ya kubadilishana taarifa miongoni mwa watoa maamuzi, wataalamu wa usalama na afya, waajiri na wawakilishi wa wafanyakazi na wataalamu kutoka hifadhi ya jamii duniani kote.

Malengo ya Mkutano ni:

- Kuandaa mkutano wa kubadilishana taarifa mpya na utendaji kwa lengo ya kukuza usalama na afya kazini duniani kote.
- Kuimarisha na kujenga mitandao na ushirikiano wakati wa kufanya kazi ya msingi kwa ajili ya ushirikiano na kuimarisha uhusiano miongoni mwa wote wanaohusika.
- Kutoa jukwaa kwa ajili ya kuendeleza maarifa, mikakati na mawazo kwa vitendo ambayo yanaweza kurekebishwa kulingana na mazingira ya mahali na kuanza kutumiwa mara moja.

Programu ya siku nne inajumuisha Mkutano wa Usalama na Afya, Kikao cha pamoja, Vikao vya Kitaalamu, Mikutano ya Kanda, Makongamano, Jukwaa la Wazungumzaji, Vikao vya kujadili mabango, na vilevile Sherehe za Kimataifa za Filamu na Vyombo vya Mawasiliano.

Mkutano wa kwanza wa Usalama na Afya utafanyika siku ya ufunguzi wa Mkutano. Viongozi wa dunia waliochaguliwa wataalikwa kutafakari juu ya usalama na afya kazini kama haki ya msingi ya binadamu na kama njia ya kukua kwa uchumi na maendeleo. Lengo la mwisho ni kuongeza sifa ya usalama na afya kazini na kufanikisha maendeleo halisi ya kupunguza ajali na magonjwa kazini.

NJOO TUKUTANE SEOUL MWAKA 2008

www.safety2008korea.org

Mkutano wa Dunia unaandaliwa na Shirika la Kazi Duniani (ILO), Chama cha Hifadhi ya Jamii cha Kimataifa (ISSA) na Wakala wa Usalama na Afya Korea (KOSHA)